YFH
INTERNATIONAL

# YFH International Business Company Limited

*Agrobusiness and [illegible] Self-investment & Development*

Dar es Salaam, 25/11/2021

**KUMB NA. YFH/BC/2021/005.**

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
WILAYA YA KALIUA,
S.L.P 83,
**KALIUA.**

**YAH: YFH INTERNATIONAL BUSINESS COMPANY LIMITED KUIOMBA OFISI YA MKURUGENZI KUPITISHA NA KUWASILISHA MAOMBI YA ARIDHI HEKARI 6000 KWAAJILI YA UWEKEZAJI WA KILIMO KWA KAMISHINA MSAIDI WA ARIDHI MKOA WA TABORA.**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

2. Kampuni ya YFH International Business Company Ltd, ni Kampuni inayotarajia kufanya shughuli zake za kilimo cha mazao ya chakula na Biashara ndani na nje ya Tanzania.

3. Kampuni hii, Ni Kampuni inayomilikiwa na Muwekezaji kutoka nje ya nchi iliyosajiliwa nchini Tanzania kwa usajili wa **BRELA No. 151024734** na kutekeleza majukumu yake ya kampuni kama ilivyoonyeshwa katika Memorandum of understanding na Article of Association.

4. Kwakuwa, kwa mujibu wa sheria ya Ardhi ya kijiji namba **5** ya **1999**, na kanuni za **2001** na tangazo la serikali namba **86** la tarehe **4/5/2001** fungu la **76** **(1)**, **(2)** na (3) hususani kifungu kidogo cha **(3)** kinachosema "Where on application is made whether by way of a customary right of occupancy or by way of a derivative right or consent to the grant of a derivative right which is greater than fifty hectares in extent, the village council shall forward, that application to the commissioner together with its recommendation on the that application and shall not grant that application unless and until the commissioner shall signify in writing to the village council that he consents to that application"

5. Kwamba, kwakuwa kikao cha maendeleo (WDC) kata ya Ugunga pamoja na Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Limbula uliridhia kuwepo na kutoa aridhi yenye ukubwa wa **ekari 6000** kwa ajili ya shughuli ya uwekezaji wa kilimo kwa

kampuni ya YFH International Business Company Ltd, ikiwa ni hatua ya utangulizi wa kupata eneo la Ardhi katika kijiji cha Limbula na kisha kuniwezesha kufuata taratibu za kisheria kwa kuonana na kituo cha uwekezaji (TIC).

6. Kwamba, kwa barua hii naomba ofisi yako iidhinishe ombi hili ili niendelee na hatua za kisheria kuhusu uwekezaji kwa kupewa ridhaa ya kuendesha kilimo ndani ya kijiji chako.

Ninaambatanisha kielelezo "**A**" barua ya maombi, "**B**" muhutasari wa mkutano mkuu wa kijiji cha Limbula pamoja na "**C**" muhutasari wa kikao cha maendeleo WDC kata ya Ugunga.

Nawasilisha.

..........................
**Boniface Habonayo**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**YFH International Business Company Ltd**

YFH INTERNATIONAL BUSINESS COMPANY LIMITED

**Nakala.**

1. MKUU WA WILAYA
   WILAYA YA KALIUA,
   S.L.P. 83,
   **KALIUA.** — Kwa taarifa.

2. KAMISHNA MSAIDIZI WA ARDHI MKOA,
   MKOA WA TABORA,
   S.L.P.342,
   **TABORA.** — Kwa taarifa.

3. MTENDAJI WA KATA
   KATA YA UGUNGA,
   S.L.P. 83,
   **KALIUA.** — Aione kwenye jalada.

Certified copy of the original
ADVOCATE NOTARY

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

Simu:+255262965679,+255262965676,+255622225618
Baruapepe: ded@kaliuadc.go.tz
Tovuti: www.kaliuadc.go.tz

S. L. P 83
Kaliua Tabora

Kumb Na. KDC/K.I/VOLIII/0387/36 20/1/2022

Kamishna wa Ardhi Msaidizi
Mkoa wa Tabora,
S.L.P. 342,
Tabora.

**YAH: MAOMBI YA ARDHI HEKARI 6000 KUTOKA YFH INTERNATIONAL BUSINESS COMPANY LIMITED**

1. Tafadhari rejea madatajwa.

2. Halmashauri imepokea na kuridhia ombi la kampuni ya **YFH INTERNATIONAL BUSINESS COMPANY LIMITED** yakutaka kuwekeza katika kilimo katika kijiji cha Limbula kilichopo kata ya Ugunga katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua. Ukubwa wa eneo wanaloomba kwa ajili ya uwekezaji huo nihekari 6000 ambazo ni zaidi ya kiwango ambacho Halmashauri inaruhusiwa kutoa. Aidha, Kijiji cha Limbula hakijapimwa na kuwekewa mpango wamatumizi bora yaardhi.

3. Kwa kuzingatia ukubwa wa eneo ambalo wawekezaji hao wameomba, nawasilisha kwako ombi lao kwa hatua zaidi.

5. Nakala ya barua yao ya maombi pamoja na mihtasari ya Kamati ya Huduma za Jamii kijiji cha Limbula, Kamati ya Uchumi, Mipango na Fedha ya Kijiji, Halmashari ya Kjiji, Kamati ya Maendeleoya Kata ya Ugunga pamoja na Mkutano wa Kijiji cha Limbula imeambatanishwa kwa wepesi wa rejea.

Nawasilisha.

*Bennet Bernard Kamara*
**KNY: MKURUGENZI MTENDAJI (W) KALIUA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 83 KALIUA

**Nakala kwa:**
Katibu Mkuu
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
S.L.P. 2908
**DODOMA.**

Certified as true copy
25/6/2022

BITAHO B. MARCO
ADVOCATE
NOTARY PUBLIC
&
COMMISSIONER FOR OATHS
DAR ES SALAAM

Katibu Mkuu
Ofisi ya Rais
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – (OR TAMISEMI)
Mji wa Serikali Mtumba
Mtaa wa TAMISEMI
S.L.P. 1923
**41185 DODOMA**.

Katibu Tawala
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P. 25
**TABORA.**

MkurugenziMtendaji,
YFH International Business Company Limited,
P. O. Box 46305,
**DAR ES SALAAM.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

*Simu: +255 26 2605546*
*Nukushi: +255 26 2605546*
*Barua pepe: acl.tabora@lands.go.tz*
*Web:www.ardhi.go.tz*

*Ofisi ya ArdhiMkoawa Tabora,*
*MtaawaShule,*
*Jengo la Ofisi la NSSF,*
*Ghorofa ya kwanza,*
*S. L. P. 342,*
*TABORA.*

*27 Januari, 2022*

Tafadhaliunapojibutaja:
***Kumb.Na. LD/WZ/0007/84***

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua,
S.L.P 83,
**Kaliua.**

**YAH:-MAOMBI YA ARDHI HEKARI 6000 KUTOKA YFH INTERNATIONAL BUSINESS COMPANY LIMITED.**

Tafadhali rejea barua yako yenye **Kumb. Na.** KDC/K.1/VOVIII/0387/36 ya tarehe 20 Januari 2022 inayohusu maombi ya ardhi kwa kampuni tajwa hapo juu.

Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Halmashauri yako kwa kuendelea kuwakaribisha wawekezaji kwenye Kilimo katika Kijiji cha Limbula Kata ya Ugunga. Aidha kwa mujibu wa taarifa tulizozipata kutoka kwa mwakilishi wa Kampuni hii Ndg. Hussein asilimia kubwa ya hisa za kampuni hii zinamilikiwa na wageni ambao sio watanzania.

Kwa mujibu wa sheria za kumiliki ardhi Taasisi/Kampuni za kigeni zitamiliki ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji na watapatiwa hatimilki isiyo ya asili (Derivative Right) kupitia kituo cha uwekezaji TIC. Aidha kwa kuwa ardhi inayoombwa ni ardhi ya kijiji taratibu za kubadilisha ardhi hiyo kutoka ardhi ya kijiji kwenda ardhi ya kawaida (uhawilishaji) zitapaswa kufuatwa na baadae ardhi hiyo itangazwe kuwa ardhi ya uwekezaji kabla haijamilikishwa kwa kituo cha uwekezaji TIC .

Hivyo tunawashauri muwajulishe wawekezaji hawa kwa kuwa tayari wamesha itambua ardhi inayowafaa kwa ajili ya uwekezaji ni vyema wakapitia kituo cha uwekezaji TIC ili waweze kujulishwa taratibu wanazopaswa kufata ili waweze kutumia ardhi hiyo kwa shughuli za uwekezaji.

Natanguliza Shukrani zangu.

E. L .Nambua
**Kny: Kamishna Msaidizi wa Ardhi**
**Mkoa wa Tabora.**

Certified as true copy of the original

Nakala:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
Mji wa serikali Mtumba,
S.L.P 2908,
**40477 - DODOMA.**

Kamishna wa Ardhi,
Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
Mji wa serikali Mtumba,
S.L.P 2908,
**DODOMA.**

Katibu Tawala Mkoa,
S.L.P 25,
**TABORA.**

Mkurugenzi Mtendaji,
YFH International Business Company Limited,
P.O.Box 46305,
**DAR ES SALAAM.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA**

**Simu:+255262965679,+255262965676,+255622225618**
**Barua pepe: ded@kaliuadc.go.tz**
**Tovuti: www.kaliuadc.go.tz**

**S. L. P 83**
**Kaliua Tabora**

Kumb. Na. KDC/M.2/0468/68

7/03/2022

MKURUGENZI
YFH International Business Company Ltd
Agrobusiness and Import-Export 4 Self-investment &Development
S.L.P.
**DAR ES SALAAM.**

**Yah: MAOMBI YA ARDHI HEKARI 6,000 KUTOKA YFH INTERNATIONAL BUSINESS COMPANY LIMITED.**

Tafadhali mada iliyotajwa hapo juu inahusika.

1. Nimepokea barua kutoka kwa Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Tabora yenye kumbukumbu namba LD/WZ/0007/84 ya tarehe 27/01/2022 ambayo inasema kuwa kwa mujibu wa Sheria za kumiliki Ardhi, Taasisi/Kampuni za kigeni zitamiliki Ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji na watapatiwa hatimiliki isiyo ya asili (Derivative Right) kupitia kituo cha uwekezaji TIC. Aidha, kwa kuwa Ardhi inayoombwa ni Ardhi ya kijiji, taratibu za kubadilisha Ardhi hiyo kutoka Ardhi ya kijiji kwenda Ardhi ya kawaida (Uhawilishaji) zitapaswa kufuatwa na baadaye Ardhi hiyo itangazwe kuwa Ardhi ya uwekezaji kabla haijamilikishwa kwa kituo cha uwekezaji TIC. .

2. Kwa kuwa tayari mmeishaitambua Ardhi inayowafaa kwa ajili ya uwekezaji. Kupitia barua hii mnaelekezwa mwende kituo cha uwekezaji TIC ili muweze kujulishwa taratibu mnazopaswa kufuata na hatimaye muweze kutumia Ardhi hiyo kwa shughuli za uwekezaji

.3. Ninakutakia utekelezaji mwema,

Kenneth Tefulukwa
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**KALIUA.**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA KALIUA
S.L.P. 83
KALIUA



Scanné avec CamScanner